

## JE, UKO KATIKA HATARI?

### I. Tathmini

Unapaswa kufanyiwa kipimo cha kifua kikuu (TB) ikiwa yoyote kati ya yafuatayo yanatumika.


Ikiwa wewe:

- ulizaliwa, umeishi (kwa zaidi ya mwezi) au umesafiri mara kwa mara katika maeneo ambayo ugonjwa amilifu wa kifua kikuu hupatikana sana - ikiwa ni pamoja na Afrika, Asia, Meksiko, Amerika ya Kati au Kusini, Visiwa vya Karibi au Ulaya Mashariki;
- umetumia muda na mtu mwenye ugonjwa amilifu wa TB;
- una na dalili za ugonjwa amilifu wa TB ikiwa ni pamoja na kikohozi ambacho kinadumu kwa wiki tatu au zaidi, homa, maumivu ya kifua, kupoteza uzito, kutokwa na jasho usiku, uchovu, au kupungua kwa hamu ya kula;
- una virusi vya ukimwi, umepandikizwa kiungo fulani cha mwili, au unatumia dawa ambazo zinadhoofisha mfumo wako wa kinga;
- unatumia dawa za kulevya kwa njia ya sindano;
- unafanya kazi au kuishi katika mazingira yenye watu wengi, kama vile makazi ya muda mfupi kwa wasio na nyumba, taasisi ya marekebisho ya tabia, au makazi ya kutunzia wakongwe na walemavu.

### 2. Pima

Hata kama hujisikii mgonjwa, bado unaweza kuwa na vimelea vya kifua kikuu katika mwili wako. Hii inamaanisha kuwa unaweza kuwa na maambukizi ya TB yasiyo na madhara na uko katika hatari ya kupata ugonjwa amilifu wa TB.

Kuna aina mbili za vipimo ambavyo vinaweza kutumika kutambua vimelea vya TB mwilini: vipimo vya damu vya TB na kipimo cha ngozi cha TB.



### 3. Tibu

Ikiwa kipimo chako kina matokeo chanya, mtoa huduma wako wa afya atakuagiza kipimo cha picha ya eksirei ya kifua chako.

Ikiwa una maambukizi ya TB yasiyo na madhara, tumia dawa aliyoagiza daktari ili kujikinga dhidi ya kupata ugonjwa amilifu wa TB ambao unaweza kuathiri familia yako, marafiki, na jamii.



Latent TB. Active Concern.  
Tuberculosis Program

